

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.CDC/A.10/17/VOL III/4

13 Julai 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI DEREVA II

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino anakaribisha maombi ya Kazi kutoka kwa Watanzania wenye Sifa na Uwezo wa Kujaza nafasi ya **Dereva II** Tangazo hili ni baada ya kupokea barua ya Kibali cha Ajira Mbadala chatarehe **23/06/2022** yenye **Kumb.Na.FA.170/360/01/42** kutoka kwa Katibu Mkuu, OR – UTUMISHI.

1. DEREVA II NAFASI 3

1.0 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe amehitimu Kidato cha IV
- ii. Leseni ya Daraja C ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda wa mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali
- iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Ufundi Stadi VETA au chuo kingine kinachotambulika na serikali
- iv. waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza

MAJUKUMU.

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari zao za kikazi
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- vi. Kufanya usafi wa gari na kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

1.1 MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Serikali TGS. B

2. MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania mwenye Umri kuanzia miaka 18 na asizidi miaka 45.
- ii. Mwombaji awasilishe Picha moja ya hivi karibuni (passport size).
- iii. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (referees) wa kuaminika.
- iv. Waombaji wote waambatanishe nakala ya Vyeti halisi vya Masomo na Taaluma masomo na transcript ya cheti cha Taaluma, Cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha "Result Slip", "Statement of Results", "Provisional Results" au "Transcript" bila nakala halisi ya Cheti cha Taaluma maombi yake hayatakubaliwa.
- v. Kwa waliosoma Nje ya Nchi Elimu ya Kidato cha nne na Kidato cha Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- vi. Wote watakoachaguliwa kufanya usaili ndio watakaoitwa kwenye Usaili (Interview).
- vii. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa.
- viii. Maombi yaandikwe kwa Mkono na yatumwe kwa Njia ya Posta kupitia Anwani iliyotajwa hapo chini.
- ix. Awe ambaye hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- x. Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe: 26/07/2022**

MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino,
S.L.P. 1126,
CHAMWINO – DODOMA.

TANGAZO hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino:www.chamwinodc.go.tz



Dkt. Semistatus .H. Mashimba,
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri,
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO
S. L. P. 1126
DODOMA